

STIISSII

majira

HABARI

Jumatatu Machi 4, 2013

5

Wakulima wadogo wapewa somo

SERIKALI imetakiwa kuweka kipaumbele katika sekta ya Kilimo Hai ambacho kinaweza kuwakwamua wakulima wadogo ambao wapo zaidi ya asilimia 70 ya wakulima wote nchini, anaripoti Christina Mokimirya.

Mwito huo ufitolewa na Mkurugenzi wa Kilimo Endelevu (SAT) Mkoa wa Morogoro, Janet Maro, alipozungumza na gazeti hili kuhusu maendeleo ya Kilimo Hai kwa nchi zinazoendelea hasa Tanzania.

Alisema Kilimo Hai uzalishaji wake ni nafuu kwa sababu malighafi ambazo zinatumiwa shambani hupatikana kwenye mazingira yanayomzunguka mkulima, kama mimea na masalia ya mimea ambayo yapo kila mahali hivyo kutumia kutengeza mbolea na dawa za kudhibiti wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea.

Alisema kilimo hicho kitamsaidia mkulima kulima kilimo endelevu, kwani hatakuwa na haja ya kutegemea kununua pembejeo kutoka nje au kusubiri apewe ruzuku na Serikali.

"Sekta ya kilimo Hai inakuwa kwa kasi nchini na duniani, tunashuhudia jinsi ambavyo watu wanatafuta vyakula vilivyolimwa bila kutumia sumu wala mbolea za chumvichumvi," alisema.

Alisema uchumi wa Tanzania unakua kwa kasi lakini mkulima mdogo bado haoni ukuaji huo, hivyo kuboresha Kilimo Hai kutasaidia mkulima mdogo kujikwamua.